SALZBURG GLOBAL SEMINAR

EDUCATION FOR TOMORROW'S WORLD

Kauli ya Salzburg
kuhusiana na Ulimwengu wa Wingi-lugha

Katika ulimwengu wa sasa wenye mahusiano mengi, uwezo wa kuzungumza lugha nyingi na kuwasiliana na watu wanaotumia lugha mbalimbali ni stadi muhimu sana. Hata ujuzi mdogo tu wa lugha zaidi ya moja ni muhimu. Ustadi katika- lugha zaidi ya moja ni aina mpya ya elimu ulimwenguni. Uwezo wa kujifunza lugha unapaswa kupanuliwa kwa wote – wachanga kwa wazee.

Hata hivyo, mamilioni ya watu kote ulimwenguni wamenyimwa haki ya kudumisha, kufurahia na kukuza lugha zao za utambulisho na za jamii. Ukosefu huu wa haki unapaswa kurekebishwa kupitia sera za lugha zinazounga mkono kuwepo kwa jamii na watu wenye ujuzi wa kiwingi-lugha.

Sisi, washiriki katika kikao cha Salzburg Global Seminar kuhusu *Jukwaa la kuboresha Vipaji: Kujifunza na Kushirikisha lugha katika Ulimwengu wa Kiutandawazi* (Disemba 12-17, 2017 salzburgglobal.org/go/586), tunasisitiza kuwepo kwa sera zinazothamini na kuendeleza kuwepo kwa wingi-lugha na haki za lugha.

Kauli ya Salzburg Kuhusiana na Ulimwengu wa Wingi-lugha itatiwa nguvu na ripoti ya kina pamoja na blogu kuhusu mada muhimu zitakazochapishwa katika mwaka wa 2018.

TUNAISHI KATIKA ULIMWENGU AMBAPO:

- Mataifa yote 193 ya Umoja wa Mataifa pamoja na watu wengi wana ujuzi wa kiwingi-lugha.
- Lugha 7,097 zinazungumzwa kote ulimwenguni hivi sasa.
- 2,464 kati ya lugha hizo zimo hatarini[1].
- Lugha 231 zinatawala, huku zikizungumzwa na zaidi ya nusu ya watu walio ulimwenguni.
- Asilimia 40% ya watu hawawezi kupata elimu katika lugha wanayoielewa[2].
- Watoto na vijana wadogo milioni 617 hawafikii kiwango cha chini cha ustadi wa kusoma unaohitajika[3].
- Watu milioni 244 ni wahamiaji wa kimataifa, watu milioni 20 kati yao ni wakimbizi, idadi iliyoongezeka kwa asilimia 41 tangu mwaka wa 2000[4]. Idadi ya wahamiaji na wakimbizi pekee inaweza kuwa sawa na idadi ya watu katika nchi ya 5 yenye watu wengi zaidi ulimwenguni[5].

Kwa kweli ulimwengu wetu ni wa wingi-lugha, japo mifumo mingi ya kielimu na kiuchumi, michakato ya kiuzalendo na tawala za umma huwatenga mamilioni ya watu kwa sababu ya lugha zao na uwezo wao wa kilugha. Ni lazima tukabiliane na changamoto hii ikiwa tunataka kufikia Malengo ya Maendeleo ya Kudumu[6], yaliyopitishwa mwaka wa 2015 na mataifa 193 ili "kumaliza umaskini, kulinda sayari hii na kuhakikisha mafanikio kwa kila mtu." Mfumo wa elimu wenye haki ambao msingi wake ni sera thabiti za lugha zisizobagua ni muhimu katika kuhakikisha maendeleo inayojumisha wote.

KANUNI

- Wingi-lugha ni dhana inayoashiria ile hali wazi ya kufundisha lugha, na vilevile
  ruwaza zisizo rasmi za mawasiliano zinazojitokeza katika jamii zilizo na wingi-lugha.
- Wingi-lugha ni ile hali ya watu kuwa na ujuzi wa lugha nyingi.
- Hali za kihistoria, kijiografia na kiuchumi-jamii husababisha aina tofauti na matumizi ya wingi-lugha.
- Elimu ya kiwingi-lugha, na kuungwa mkono kwa wingi-lugha katika jamii kunakofanywa na mataifa
  pamoja na mashirika ya kimataifa, hukuza ubadilishanaji wa ujuzi na uelewa wa tamaduni mbalimbali na huimarisha mahusiano ya kimataifa.

wa zinaweza kuimarisha mshikamano wa jamii, kuboresha matokeo ya elimu na iuchumi. Mielekeo ya kimasomo ya kufahamu lugha zaidi huwaruhusu watoto

The *Salzburg Statement for a Multilingual World* was jointly drafted in English by Salzburg Global Fellows. All translations have been provided through the goodwill and voluntary efforts of the Fellows and their colleagues. Read the original here: education.salzburgglobal.org/statements

kujenga ustadi mkubwa wa kusoma na kuandika katika lugha zao za mama; huwasaidia wanajamii kudumisha lugha zao za kujitambulisha, ujuzi na imani; na hutoa nafasi za kujifunza lugha mpya kwa manufaa ya kibinafsi, burudani, utamaduni au ya kiuchumi. Sera za kiwingi-lugha zinaweza kudumisha raslimali muhimu na ya kipekee ya utofauti katika lugha na kuendesha mabadiliko mazuri ulimwenguni, kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Tunawahimiza watu, mashirika, taasisi na serikali mbalimbali kuendeleza mtazamo wa kiwingi-lugha unaounga mkono kuwepo kwa lugha nyingi kama hali ya kawaida ulimwenguni, na unaokabiliana na ubaguzi wa lugha, na kukuza sera za lugha zinazoendeleza wingi-lugha.

MAPENDEKEZO

Uundaji wa Sera

Sera ya lugha itakayofanikiwa inahitaji mchango kutoka kwa wataalamu na ushirikisho wa moja kwa moja wa washikadau kutoka kwenye jamii. Kufanya maamuzi wazi na yasiyo na mapendeleo kuhusu lugha kuna maana ya:

- Kufanya mashauriano kuhusu malengo wazi yanayoweza kutekelezwa na kufikiwa.
- Kuwajumuisha washikadau wote katika mchakato wa kuunda sera, huku walimu wakipewa jukumu muhimu katika hatua zote.
- Kupanga sera kutoka kipindi cha kabla ya shule hadi baada ya shule na vilevile elimu isiyo rasmi na ya maishani mwote.
- Kulenga vipengele na mahitaji yote ya lugha, ikiwemo udumishaji, ujifunzaji na matumizi ya lugha za kwanza za jamii za walio wachache.
- Kutumia maono kutoka kwa utafiti wa kielimu na kimantiki kuhusiana na ujifunzaji wa lugha za mama na lugha nyinginezo.
- Kutumia uwezo wa teknolojia za mawasiliano.
- Kutafuta raslimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji kamili wa sera.
- Kufuatilia na kutathmini malengo ya sera na utekelezaji wake mara kwa mara.

Kufundisha na Kujifunza

Upeo kamili wa sera ya lugha ni jamii, uchumi na utamaduni na vile vile elimu. Kujifunza lugha katika hatua zote za maisha katika jamii ni muhimu ili kudumisha na kunufaika kutokana na wingi-lugha. Sera za elimu, stadi na kazi zinapaswa kukuza na kutambua mafunzo ya lugha kwa wote, pamoja na kuthamini tofauti zilizopo kati ya lugha mbalimbali. Watoto na watu wazima wanapaswa kufikia nafasi zilizoshirikishwa na zisizo koma za kukuza, kuimarisha na kupanua uwezo wao wa lugha katika maisha yao yote.

Kielelezo kipya cha elimu kinahitajika kinayojumuisha mfumo wa kijadi na mifumo mingine mbadala ya kiujuzi na kilicho na uwezo wa kutumia teknolojia za kisasa vilivyo. Maeneo ya kujifunza lugha hayapatikani tu shuleni na katika taasisi za elimu ya juu. Mitaani, nyumbani, mitandao ya kijamii, mazingira ya kidijitali, na sehemu wanakosaidiwa wakimbizi, yote ni maeneo ambapo kujifunza na kuthamini lugha kunaweza kuendelezwa.

Tafsiri na Ukalimani

Huduma hizi ni muhimu sana katika kusanifu na kuwasilisha huduma za umma na katika kubadilishana taarifa katika jamii za wingi-lugha. Ushirikiano wenye usawa katika mazingira ya afya, elimu, uchumi na sheria hutegemea upatanisho wa lugha wa kitaalamu na unaopatikana kwa namna huru.

WITO WA KUCHUKUA HATUA

Washikadau wanaoweza kuendesha mabadiliko ni pamoja na watafiti na walimu; wafanyakazi wa jamii, asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali; walio na sauti ya kitamaduni na vyombo vya habari; maafisa wa serikali na wa umma; wanabiashara; makampuni ya msaada na maendeleo; na wakfu mbalimbali na asasi za udhamini. ***Tunatuma wito kwao wote ili wasaidie:***

- Kukuza sera za lugha, desturi na teknolojia zinazohimiza jamii thabiti na zenye mshikamano zilizo na mitazamo bora kuhusianana wingi-lugha.
- Kuhimiza kikamilifu haki za lugha, wingi wake na uzalendo kwenye stakabadhi rasmi na ujumbe kwa umma.
- Kukabiliana na hali zote za ubaguzi, mapendeleo, uonevu na ukosefu wa usawa unaohusishwa na lugha na ujuzi wa kusoma na kuandika.
- Kutambua kuwa walio wachache, wahamiaji na wakimbizi wana uwezo mkubwa wa kiisimu ambao una thamani kubwa katika ulimwengu wetu wa sasa na wa siku za usoni.

Katika njia zao za kipekee, kila mojawapo wa vikundi hivi vya washikadau vinaweza kukubali na kuhimiza wingi-lugha kwa ajili ya maendeleo ya jamii, haki za jamii na uzalendo shirikishi. Pamoja, tunaweza kuchukua hatua ili kulinda hazina ya utamaduni na ujuzi ya wingi-lugha kwa ajili ya vizazi vijavyo.

1 Kitabu cha Ramani ya Lugha, UNESCO: http://www.unesco.org/languages-atlas/

2 "Asilimia 40 ya watu hawawezi kupata elimu katika lugha wanayoielewa," UNESCO: https://en.unesco.org/news/40-don-t-access-education-language-they- understand

3 "Watoto na vijana wadogo milioni 617 hawafikii kiwango cha chini cha ustadi wa kusoma na hisabati unaohitajika," UNESCO: https://en.unesco.org/news/617- million-children-and-adolescents-not-getting-minimum-reading-and-math

4 Ripoti ya Uhamiaji ya Ulimwengu, 2015, Shirika la Uhamiaji la Kimataifa: https://www.iom.int/world-migration-report-2015

5 Uhusiano wa Idadi ya Watu, Nchi Nambari Tano katika Ukubwa: http://www.populationconnection.org/article/fifth-largest-country/

6 Malengo ya Maendeleo ya Kudumu, Umoja wa Mataifa http://www.un.org/sustainabledevelopment/sustainable-development-goals/